
hamiaji kuwa amiaji. kuboresha ofisi zake, ambapo karibu vyombo vyote "Kiwanda hicho hivi sasa kinatengeneza "crown', zikitumika tangu baada ya Uhuru hadi sasa.

HABARILEO UK 7.

# Mifugo kuendeshwa kibiashara, uvuvi kusimamiwa vyema

**Na Anastazia Anyimike, Dodoma**



WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imejipanga kuhakikisha sekta ya mifugo inaendeshwa kibiashara zaidi ili kuleta tija kwa wafugaji na taifa kwa ujumla.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (pichani) wakati wa kuelezea mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi ndani ya miaka 60 ya Uhuru.

Alisema wizara itahakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinasimamiwa ipasavyo ili kuwa na uvuvi na ukuzaji wa viumbe-maji endelevu, maendeleo ya viwanda, ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla.

Alifafanua kwamba serikali inalenga ushirikiano na wadau mbalimbali wa sekta binafsi ili kukuza na kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa kasi zaidi.

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, Ndaki alisema imefanya tathmini ya mahitaji ya samaki nchini ambapo makadirio ni tani 750,000 kwa mwaka ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 496,390, sawa na upungufu wa tani 253,615.

Alisema kiwango cha ulaji wa samaki kwa sasa ni kilo 8.5 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na kiwango kinachopendekezwa na Shirika na Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) cha kilo 20.3 kwa mtu kwa mwaka.

"Juhudi zinazoendelea za kuongeza uzalishaji wa samaki nchini zitaongeza ulaji wa samaki kwa Watanzania kufikia kilo 10.5 ifikapo mwaka 2026," alisema.

Aliainisha kuwa katika eneo la uvuvi kwenye maji asili wanatarajia kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi kutoka tani 473,592 mwaka 2020 hadi tani 600,000 ifikapo Juni 2026 kwa kuimarisha miundombinu ya uvuvi, kujenga na kukarabati mialo, masoko na kuboresha teknolojia za uhifadhi ili kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kutoka asilimia 30 hadi asilimia 10 baada ya kuvunwa.

Pia kuhamasisha teknolojia sahihi za uvuvi na matumizi ya zana bora kwa wavuvi wadogo kutoka vyombo 13,593 vinavyotumia injini hadi vyombo 25,000.

Hatua nyingine alisema ni kujenga bandari ya uvuvi na kununua meli nne za Shirika la Uvuvi la Taifa (TAFICO) ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ).

Alisema pia serikali inajipanga kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95.

"Lakini pia tutaongeza maeneo ya uhifadhi wa mazalia na makulia ya samaki kutoka asilimia moja hadi asilimia 10 kwenye maji ya bahari na maziwa," alisema.

Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Kahama mkoani Shinyanga. (Picha na Wizara ya Ardhi).

MZALENDO UK 20

# *Ulega aagiza uzalishaji nyavu bora uvuvi dagaa*

**Na JOHARI SHANI,** *Mwanza*

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekitaka kiwanda cha kuzalisha nyavu za kuvulia dagaa cha Ziwa Net, kuzalisha nyavu hizo kwa kuzingatia ubora.

Ulega aliyasema hayo wakati alipotembelea kiwanda cha Ziwa Net kilichopo Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza kwa lengo la kuona namna uzalishaji wa nyavu hizo unavyokwenda ambapo uongozi wa kiwanda hicho umetakiwa kuzingatia ubora katika uzalishaji wa nyavu na kuhakikisha wanazalisha nyavu za kutosha ili wavuvi wasipate shida kuzitafuta.

Pia, Ulega alimpongeza mwekezaji huyo wa Kiwanda cha Ziwa Net kwa uamuzi wake wa kujenga kiwanda na kutoa ajira nyingi kwa wanawake kwani kati ya waajiriwa 18, wanawake ni 15.

Naibu Waziri Ulega aliwasihi kuhakikisha wanazingatia misingi ya ajira bila unyanyasaji wa watumishi na kuendelea kuwekeza katika utengenezaji wa nyavu za aina nyingine zikiwemo za kuvulia samaki na nyavu maalumu za kutengenezea vizimba vya samaki.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, alisema uwepo wa kiwanda hicho ni muhimu sana kwa wavuvi kwani itawarahisishia upatikanaji wa nyavu kwa bei nafuu na itapunguza uvuvi haramu.

Meneja Masoko wa Kiwanda cha Ziwa Net, Christina Melkiadi, alisema lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hicho ni kurahisisha upatikanaji nyavu za dagaa kwa wavuvi, kukuza na kutangaza zana bora za uvuvi na kufungua fursa za ajira kwa vijana watakaoajiriwa katika kiwanda hicho.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha vipande 66 vyenye urefu wa mita 75 na upana wa mita 3.2 kwa siku, ambapo uzalishaji kwa mwezi ni vipande 2,000 ikiwa ni nyavu zenye ubora unaotakiwa na matundu ya kipenyo cha ukubwa wa milimita nane kama sheria inavyoelekeza.

**NYAVU**

## UBORA

Aliwasihi kuhakikisha wanazingatia misingi ya ajira bila unyanyasaji wa watumishi na kuendelea kuwekeza katika utengenezaji wa nyavu za aina nyingine zikiwemo za kuvulia samaki...

Scanned with CamScanner